

Afya yafia wapi?



Afya?



Jishindie kompyuta
ndani!

Afya yafia wapi?



Afya?



Jishindie kompyuta
ndani!

Kijitabu hiki kimetaryishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:

Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:

Daniel Mzena

Wahariri:

Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na Justice Rutenge

Usanifu:

Winston Churchill Shauri



©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255 719 751 928

+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com

wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Tumezoea kuona kwamba afya ni ukosefu wa magonjwa tu. Kama mtu haumwi, basi ana afya nzuri. Lakini afya ina maana pana zaidi ya hapo. Sera ya Taifa ya Afya inatambua kwamba afya ni:

Hali ya uzima kamili, kimwili, kiakili na kijamii.

Uzima kimwili inaeleweka kwa urahisi. Kama hatuumwi au hatujaumia, kama miili yetu imekaa sawa, tunao uzima kimwili.

Uzima kiakili ni hali ya kujitambua, vipaji vyetu, udhaifu wetu na nafasi yetu katika jamii, pamoja na kuweza kupanga malengo yetu katika maisha kulingana na kujitambua hivyo. Ni kuwa makini pia katika kazi na maisha yetu ili kuyafikia hayo malengo. Ni hali ya kujiendeleza kielimu na kupanua uelewa na stadi za maisha ili kuweza kuchambua maisha yetu na mazingira yetu kwa kina na kuondoa fikra finyu au kutawaliwa na mihemko.

Uzima kijamii ni uwezo wa kujenga mahusiano mema na watu katika jamii, pamoja na kuweza kuishi vema kulingana na mila na desturi zake. Hii haina maana kwamba lazima mtu afuate kila kitu, lakini anajua pia jinsi ya kuwashawishi watu kuboresha au kubadilisha yale yanayohitaji kubadilishwa.

Hivyo afya yetu hutegemea sana mazingira tunamoishi. Hata serikali imetambua hiyo kwa kuunganisha sekta za Afya na Ustawi wa Jamii katika Wizara moja. Jamii inayokosa ustawi itakuwa na matatizo mengi ya afya kiakili na kijamii.

Ndiyo maana, tukitaka watoto na vijana wetu wakue vema, haitoshi kupunguza magonjwa tu bali hatuna budi kuhakikisha kwamba mazingira yanawajenga kiakili na kijamii pia.

- Mazingira ya shule yawe ya kuwaelimisha watoto na vijana si ya kuwakatisha tamaa. Kuwaacha vijana wakae wenyewe bila shughuli muda mrefu ni chanzo kikubwa sana cha kuharibika kwao.
- Mazingira ya jamii yawe ya kuhakikisha vijana wote wanaweza kupita kwa usalama, wakati wowote, bila kutishwa, au kunyanyaswa kijinsia. Kitendo cha kunyanyaswa kijinsia kinawenza kumwathiri msichana au mvulana kiakili na kijamii maisha yake yote.
- Hali ya jamii iwe ya kujenga matumaini ya kufanikiwa katika maisha. Kukaa bila ajira na bila uwezo wa kujiajiri nayo inawaathiri sana vijana, ndiyo maana wengi wanaanza kuijingiza katika matumizi ya dawa za kulevya, au vitendo vya uhalifu.
- Uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya familia na jamii ni kigezo kimoja muhimu cha afya maana kadiri mtu anavyoshiriki, na kuthaminiwa katika kushiriki kwake, anakua sana kiakili na kijamii. Ndiyo maana vijana wengi wamechoka na kujitenga na jamii zao maana wanaona kwamba hawathaminiwi kabisa.
- Michezo na burudani zingine huwapatia vijana nafasi ya kuimarisha afya zao kimwili lakini pia kujenga afya yao kijamii, kwa mfano kucheza kwa pamoja kunajenga ushirikiano.

Kwa vigezo hivyo, tunaonaje hali ya vijana na watu wengine katika jamii zetu, kimwili, kiakili na kijamii?

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

Wahusika



Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bonge:



Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Bibiye:



Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mwenyekiti:



Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Mtendaji:



Mtaalamu wa afya kutoka wilayani

Bwana Afya:




Tunataka kijiji chetu
kiwe mfano wa kuigwa
Kwenuye afya. Hivi
karibuni tutaanza
kampeni ya afya.
Na hiyo ni kazi yenu
vijana.



Tunamkaribisha
Bwana Afya ili
azungumze
nanyi.

Kwanza lazima
tujipongeze hapa katani.
Tumepiga hatua kubwa
sana. Tumepunguza
magonjwa ya maambukizo.



Nikukatishe kidogo
mtaalamu, unaona
hata afya za vijana
zimekuwa nzuri...

... mnakula vizuri,
mnalala pazuri. Si
unamwona Bonge?

Huu mwili
mkubwa tu mzee
sio afya.

Tunataka
kuhamasisha watu kunawa
mikono kwa sabuni kila
mara. Na hii ni muhimu
Sana katika kukomesha
magonjwa ya kuhara.

Mpo tayari kwa
kazi vijana?

Kulikoni.
Hantaki?



Ni Kweli magonjwa
yamepungua. Lakini
kupungua kula magonjwa
peke yake ni afya
bora?

Ohoo! Nilijuatu.
Hizi stadi za maisha
Zime wafanya
wabishi kama...

Subiri. Mna
maana gani
Vijana?

Mazingira yetu
Yanadhoofisha
afya.

Nini tena?
Mbona tunaondoa
mazalia ya
Mbu!

Si hiyo tu.
Tuko tayari lakini
hebu turuhusu
tuwatembeze
kidogo leo au kesho.

Tuwaonyeshe
afya inapofia.
Kisha
tuzungumzie
mambo ya
kunawa mikono



Kesho yake

Haya ni maji
yetu ya konywa.

Hata kiwa Sabuni
utakuwa unachafua
mikono badala
ya kusafisha.

Labda tonywe
maji na
Sabuni ndio
itasafisha
tumbo!?




Afya si pamoja
na afya ya
akili na roho
pia?

Kabisa.
Ni muhimu sana
pamoja na
afya ya kijamii.

Enhee!
Papohapo. Hebu
tuone. Kama
shule inaleta
afya hizo?



















Baada ya wiki mbili



Bange yuko kempu na vijana

Michezo jamani. Kwa
nini tusianzishe
mashindano ya vitongoji?

Lakini tutapata
wapi mpira?
Na jezi? Na...

Acheni hizo. Mimi
nitatoa mpira miwili.
Changamkeni na wengine
watachangia. Kila siku
kutegemea msaada tu,
sio afya.



Kweli
mwana. Hebu
tujaribu.

Tuanzishe chama
letu la kijiji' na
Bonge atakuwa
kipa.

Haupiti
mpira,
hapo!



Kisimani

He kumbe
nyie Vijana
mnaweza.

Tunaweza sana.
Lakini hii ni kazi
rasmi. Tulipeni
sisi Vijana
kidogo tufanye
kila mara.







Na mimi nimeongea
na halmashauri, Vijana
mpate mikopo na
msaada mwiningine.
Mmekuwa mfano
kwa Wote.

Hapo sasa.
Tukiwa na miradi
yetu ni afya pia.

Na kujepusha
na mambo
mengine.

Na huu ni michango
wa Sabuni kutoka kwa
wafanyakishara ili
vyoo vya Ofisi na shule
viwe mfano bora wa
kuhawa mikono.



Je wajua?

1. Mpango wa MKUKUTA unalenga uboreshaji wa hali ya maisha na uzima wa kijamii inayounganisha elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama, usafi wa mazingira, makazi bora na matumizi endelevu ya mazingira. Lakini:
 - a. Matatizo ya uhaba wa walimu, zana na vitabu mashulenii yanaathiri maendeleo (ki-afya) ya wanafunzi. Hali hii ni mbaya zaidi katika shule za kata.
 - b. Idadi ya wasiojua kusoma na kuandika inazidi kupanda na kufikia 31% mwaka 2010. Asilimia 19 ya wanawake na 9.5% ya wanaume (wenye umri kati ya miaka 15 na 49) hawaajaenda shule.
 - c. Idadi ya wasichana wanaoacha shule kwa sababu ya kupata mimba inazidi kuongezeka na kufikia 10.3% mwaka 2008. Hali hii inaendana na matatizo ya kupanga chumba ili waende shule pamoja na unyanyasaji kijinsia | ulioshamiri.
 - d. Ukocefus wa chakula shulenii unaathiri uwezo wa wanafunzi kusoma na kukua.
 - e. Asilimia arobaini ya watu vijijini hawana maji safi na salama, hivyo wasichana na wanawake wanalazimika kupteza muda mwingu na pia kuwa hatarini kunyan-yaswa kijinsia.
 - f. Chini ya robo ya kaya zina vyoo bora. Aidha taasisi rasmi hazionyeshi mfano mzuri wa vyoo safi. Kwa mfano mashulenii, kwenye vituo vy ya afya, sokoni na maofisini.
 - g. Ingawa zaidi ya 5% ya watu wana ulemavu, huduma kwa walemovu bado ni haba.
2. Katika tafiti za TAMASHA wasichana wengi hulazimika kutafuta wapenzi ili wachangie matumizi ya nyumbani.



Tumezoea kuwalaumu watoto na vijana kwamba wana tabia mbaya lakini:

- Katika jamii yetu, tumechunguza jinsi mazingira yanavyoathiri ukuaji na uzima wa watoto na vijana wetu?
- Hali ikoje?
- Tumefanya nini kurekebisha hali hii?

Shindano

Toa maoni, jishindie kompyuta!

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenvye vitabu na tovuti.

Sharti: Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013

Anuanı: OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua pepe: unaselamej@gmail.com

Kumbuka kuweka taarifa hizi:

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership - OGP).

**Open
Government
Partnership**

Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendeleza uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.

Kijitabu hiki kimetaryishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:

Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:

Daniel Mzena

Wahariri:

Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na
Justice Rutenge

Usanifu:

Winston Churchill Shauri



©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255 719 751 928

+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com

wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Tumezoea kuona kwamba afya ni ukosefu wa magonjwa tu. Kama mtu haumwi, basi ana afya nzuri. Lakini afya ina maana pana zaidi ya hapo. Sera ya Taifa ya Afya inatambua kwamba afya ni:

Hali ya uzima kamili, kimwili, kiakili na kijamii.

Uzima kimwili inaeleweka kwa urahisi. Kama hatuumwi au hatujaumia, kama miili yetu imekaa sawa, tunao uzima kimwili.

Uzima kiakili ni hali ya kujitambua, vipaji vyetu, udhaifu wetu na nafasi yetu katika jamii, pamoja na kuweza kupanga malengo yetu katika maisha kulingana na kujitambua hivyo. Ni kuwa makini pia katika kazi na maisha yetu ili kuyafikia hayo malengo. Ni hali ya kujiendeleza kielimu na kupanua uelewa na stadi za maisha ili kuweza kuchambua maisha yetu na mazingira yetu kwa kina na kuondoa fikra finyu au kutawaliwa na mihemko.

Uzima kijamii ni uwezo wa kujenga mahusiano mema na watu katika jamii, pamoja na kuweza kuishi vema kulingana na mila na desturi zake. Hii haina maana kwamba lazima mtu afuate kila kitu, lakini anajua pia jinsi ya kuwashawishi watu kuboresha au kubadilisha yale yanayohitaji kubadilishwa.

Hivyo afya yetu hutegemea sana mazingira tunamoishi. Hata serikali imetambua hiyo kwa kuunganisha sekta za Afya na Ustawi wa Jamii katika Wizara moja. Jamii inayokosa ustawi itakuwa na matatizo mengi ya afya kiakili na kijamii.

Ndiyo maana, tukitaka watoto na vijana wetu wakue vema, haitoshi kupunguza magonjwa tu bali hatuna budi kuhakikisha kwamba mazingira yanawajenga kiakili na kijamii pia.

- Mazingira ya shule yawe ya kuwaelimisha watoto na vijana si ya kuwakatisha tamaa. Kuwaacha vijana wakae wenyewe bila shughuli muda mrefu ni chanzo kikubwa sana cha kuharibika kwao.
- Mazingira ya jamii yawe ya kuhakikisha vijana wote wanaweza kupita kwa usalama, wakati wowote, bila kutishwa, au kunyanyaswa kijinsia. Kitendo cha kunyanyaswa kijinsia kinawenza kumwathiri msichana au mvulana kiakili na kijamii maisha yake yote.
- Hali ya jamii iwe ya kujenga matumaini ya kufanikiwa katika maisha. Kukaa bila ajira na bila uwezo wa kujiajiri nayo inawaathiri sana vijana, ndiyo maana wengi wanaanza kuijingiza katika matumizi ya dawa za kulevya, au vitendo vya uhalifu.
- Uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya familia na jamii ni kigezo kimoja muhimu cha afya maana kadiri mtu anavyoshiriki, na kuthaminiwa katika kushiriki kwake, anakua sana kiakili na kijamii. Ndiyo maana vijana wengi wamechoka na kujitenga na jamii zao maana wanaona kwamba hawathaminiwi kabisa.
- Michezo na burudani zingine huwapatia vijana nafasi ya kuimarisha afya zao kimwili lakini pia kujenga afya yao kijamii, kwa mfano kucheza kwa pamoja kunajenga ushirikiano.

Kwa vigezo hivyo, tunaonaje hali ya vijana na watu wengine katika jamii zetu, kimwili, kiakili na kijamii?

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

Wahusika



Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bonge:



Mwelimidhaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Bibiye:



Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mwenyekiti:



Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Mtendaji:



Mtaalamu wa afya kutoka wilayani

Bwana Afya:




Tunataka kijiji chetu
kiwe mfano wa kuigwa
kwenuye afya. Hivi
karibuni tutaanza
kampeni ya afya.
Na hiyo ni kazi yenu
vijana.



Tunamkaribisha
Bwana Afya ili
azungumze
nanyi.

Kwanza lazima
tujipongeze hapa katani.
Tumepiga hatua kubwa
sana. Tumepunguza
magonjwa ya maambukizo.



Nikukatishe kidogo
mtaalamu, unaona
hata afya za vijana
zimekuwa nzuri...

... mnakula vizuri,
mnalala pazuri. Si
unamwona Bonge?

Huu mwili
mkubwa tu mzee
sio afya.

Tunataka
kuhamasisha watu kunawa
mikono kwa sabuni kila
mara. Na hii ni muhimu
Sana katika kukomesha
magonjwa ya kuhara.

Mpo tayari kwa
kazi vijana?

Kulikoni.
Hantaki?



Ni Kweli magonjwa
yamepungua. Lakini
kupungua kula magonjwa
peke yake ni afya
bora?

Ohoo! Nilijuatu.
Hizi stadi za maisha
Zime wafanya
wabishi kama...

Subiri. Mna
maana gani
Vijana?



Kesho yake

Haya ni maji
yetu ya konywa.

Hata kiwa Sabuni
utakuwa unachafua
mikono badala
ya kusafisha.

Labda tonywe
maji na
Sabuni ndio
itasafisha
tumbo!?



Afya si pamoja
na afya ya
akili na roho
pia?

Kabisa.
Ni muhimu sana
pamoja na
afya ya kijamii.

Enhee!
Papohapo. Hebu
tuone. Kama
shule inaleta
afya hizo?

















Matatizo hayo ni ya
Siku nyīngi. Mpaka
tupate wafadhili.

Kungoja kuletemwa
ni Sawa na kungoja
mvua wakati
wa kiangazi.

Lakini tunaweza
kubadilisha hii hali.



Baada ya wiki mbili



Bange yuko kempu na vijana

Michezo jamani. Kwa
nini tusianzishe
mashindano ya vitongoji?

Lakini tutapata
wapi mpira?
Na jezi? Na...

Acheni hizo. Mimi
nitatoa mpira miwili.
Changamkeni na wengine
watachangia. Kila siku
kutegemea msaada tu,
sio afya.



Kweli
mwana. Hebu
tujaribu.

Tuanzishe chama
letu la kijiji' na
Bonge atakuwa
kipa.

Haupiti
mpira,
hapo!



Kisimani

He kumbe
nyie Vijana
mnaweza.

Tunaweza sana.
Lakini hii ni kazi
rasmi. Tulipeni
sisi Vijana
kidogo tufanye
kila mara.







Na mimi nimeongea
na halmashauri, Vijana
mpate mikopo na
msaada mwiningine.
Mmekuwa mfano
kwa Wote.

Hapo sasa.
Tukiwa na miradi
Yetu ni afya pia.

Na kujepusha
na mambo
mengine.

Na huu ni michango
wa Sabuni kutoka kwa
wafanyakishara ili
vyoo vya Ofisi na shule
viwe mfano bora wa
kuhawa mikono.



Je wajua?

1. Mpango wa MKUKUTA unalenga uboreshaji wa hali ya maisha na uzima wa kijamii inayounganisha elimu, afya, upatikanaji wa maji safi na salama, usafi wa mazingira, makazi bora na matumizi endelevu ya mazingira. Lakini:
 - a. Matatizo ya uhaba wa walimu, zana na vitabu mashulenii yanaathiri maendeleo (ki-afya) ya wanafunzi. Hali hii ni mbaya zaidi katika shule za kata.
 - b. Idadi ya wasiojua kusoma na kuandika inazidi kupanda na kufikia 31% mwaka 2010. Asilimia 19 ya wanawake na 9.5% ya wanaume (wenye umri kati ya miaka 15 na 49) hawaajaenda shule.
 - c. Idadi ya wasichana wanaoacha shule kwa sababu ya kupata mimba inazidi kuongezeka na kufikia 10.3% mwaka 2008. Hali hii inaendana na matatizo ya kupanga chumba ili waende shule pamoja na unyanyasaji kijinsia | ulioshamiri.
 - d. Ukocefus wa chakula shulenii unaathiri uwezo wa wanafunzi kusoma na kukua.
 - e. Asilimia arobaini ya watu vijijini hawana maji safi na salama, hivyo wasichana na wanawake wanalazimika kupteza muda mwingu na pia kuwa hatarini kunyan-yaswa kijinsia.
 - f. Chini ya robo ya kaya zina vyoo bora. Aidha taasisi rasmi hazionyeshi mfano mzuri wa vyoo safi. Kwa mfano mashulenii, kwenye vituo vya afya, sokoni na maofisini.
 - g. Ingawa zaidi ya 5% ya watu wana ulemavu, huduma kwa walemovu bado ni haba.
2. Katika tafiti za TAMASHA wasichana wengi hulazimika kutafuta wapenzi ili wachangie matumizi ya nyumbani.



Tumezoea kuwalaumu watoto na vijana kwamba wana tabia mbaya lakini:

- Katika jamii yetu, tumechunguza jinsi mazingira yanavyoathiri ukuaji na uzima wa watoto na vijana wetu?
- Hali ikoje?
- Tumefanya nini kurekebisha hali hii?

Shindano

Toa maoni, jishindie kompyuta!

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenvye vitabu na tovuti.

Sharti: Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013

Anuanı: OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua pepe: unaselamej@gmail.com

Kumbuka kuweka taarifa hizi:

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership - OGP).

**Open
Government
Partnership**



Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendezea uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.